JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Kumb. Na. **EB.32/160/01/106**

**09th February, 2024**

Wapo Mission International Company Limited,
(WAPO FM Radio),
S.L.P 6178,
**14121 DAR ES SALAAM**

## UAMUZI WA AMRI YA UTEKELEZAJI

(Umetokana na Amri ya Utekelezaji iliyotolewa kwa WAPO FM Radio tarehe 4 Januari 2024)

### 1.0 UTANGULIZI

1.1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) (**"Mamlaka"**) ilitoa leseni ya kutoa huduma za utangazaji kwa njia ya Radio jijini Dar es Salaam, kwa **WAPO FM Radio** (**"Mtoa huduma"**) mnamo tarehe 14 Julai 2015.

1.2. Mtoa huduma, anapotoa huduma za utangazaji kwa njia Radio ana wajibu wa kuzingatia na kutekeleza Sheria, Kanuni, Masharti ya Leseni na Maelekezo/Amri mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka.

1.3. Kwa mujibu wa Kanuni ya 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018 pamoja na masharti ya leseni, mtoa huduma hatakiwi kutangaza matangazo yanayohusiana na dawa za tiba asili/mbadala isipokuwa kwa idhini ya mamlaka husika yaani Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Tanzania (TAHPC).

1.4. Mnamo mwezi Septemba 2023, Mamlaka ikiwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kusimamia na kufuatilia maudhui ya vituo vya utangazaji nchini, ilibaini kwamba **WAPO FM Radio** imekiuka Kanuni na Masharti ya Leseni kwa kutangaza matangazo ya watoa huduma za tiba asili na tiba mbadala ya ***Pelegrino Investment Sanitarium Clinic***, ***Tesha Herbal Clinic& Natural Therapy*** na ***Dr. Magida Traditional Medicine*** ambayo hayajaidhinishwa na TAHPC.

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified

1.5. Tarehe 05 Oktoba, 2023, Mamlaka ilikiandikia Kituo cha **WAPO FM Radio** maelekezo ya kusitisha mara moja matangazo ya tiba asili na tiba mbadala ambayo hayana idhini ya TAHPC, yakiwemo ya ***Pelegrino Investment Sanitarium Clinic.*** Hata hivyo, **WAPO FM Radio** haikutekeleza maelekezo hayo.

1.6. Tarehe 14 Novemba, 2023, Mamlaka ilikiandikia Kituo cha **WAPO FM Radio** maelekezo ya kuwasilisha ndani ya siku tatu (3), ushahidi iwapo matangazo ya tiba asili na tiba mbadala ya ***Tesha Herbal Clinic& Natural Therapy*** ambayo walikuwa wakiyatangaza, yameidhinishwa na TAHPC. **WAPO FM Radio** haikutekeleza maelekezo hayo pia.

1.7. Ufuatiliaji ulioendelea kufanywa na Mamlaka, Mwezi Disemba 2023, umebaini kuwa **WAPO FM Radio** imeendelea kutangaza matangazo ya watoa huduma za tiba asili na tiba mbadala ambayo hayajaidhinishwa na TAHPC ambapo tarehe 19 Desemba, 2023, Saa 07:54 Mchana, **WAPO FM Radio** ilitangaza matangazo ya tiba asili na tiba mbadala ya ***Dr. Magida Traditional Medicine*** bila matangazo hayo kuidhinishwa na TAHPC.

## 2.0 AMRI YA UTEKELEZAJI

2.1 Kifungu cha 48 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, kinaipa Mamlaka ya Mwasiliano mamlaka ya kutoa kwa Mtoa huduma, Amri ya Utekelezaji ya kusitisha vitendo vya ukiukaji wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni na kumtaka kurekebisha na kuzingatia Sheria, Kanuni na Masharti ya leseni katika utoaji wa huduma yake.

2.2 Tarehe 4 Januari 2024, Mamlaka ilitoa Amri ya Utekelezaji kwa WAPO FM Radio ya kuacha mara moja kutangaza matangazo ya tiba mbadala yasiyozingatia Sheria; na kuwasilisha kwa Mamlaka maelezo kimaandishi ifikapo tarehe **18 Januari 2024** na kufika katika Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, 20 Barabara ya Sam Nujoma, tarehe **23 Januari 2024**, kutoa utetezi wake wa kwa nini hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti zisichukuliwe dhidi yake kwa: -

a) kukiuka Kanuni ya 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018 pamoja na masharti ya leseni, kwa kutangaza matangazo ya watoa huduma za Tiba Asili

na Tiba Mbadala ya ***Pelegrino Investment Sanitarium Clinic***, ***Tesha Herbal Clinic& Natural Therapy*** na ***Dr. Magida Traditional Medicine*** ambayo hayajaidhinishwa na TAHPC.; na

b) kukaidi maelekezo ya Mamlaka yaliyotolewa kwa mujibu wa Sheria.

## 3.0 KUSIKILIZWA KWA AMRI YA UTEKELEZAJI

Tarehe 18 Januari 2024, WAPO FM Radio iliwasilisha kwa Mamlaka maelezo ya kimaandishi yaliyosainiwa na Edna Malisa, Mkurugenzi wa Wapo Media na Tarehe 23 Januari 2024, WAPO FM Radio ikiwakilishwa na Edna Malisa Mkurugenzi na Benitho Mtulo, Mkuu wa Utawala, walifika katika Ofisi za Mamlaka kutoa utetezi kwanini hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti zisichukuliwe dhidi ya WAPO FM Radio. Utetezi wa WAPO FM Radio wa maandishi na njia ya mdomo umeainishwa kwenye aya ya 4.0.

## 4.0 UTETEZI WA WAPO FM RADIO

4.1 Katika utetezi wao, WAPO FM Radio walikiri kupokea Amri ya Utekelezaji ya tarehe 4 Januari 2024 kutoka kwa Mamlaka. Kwamba katika kutekeleza Amri hiyo, waliwasilisha maelezo ya kimaandishi tarehe 18 Januari 2024 na pia wamefika katika ofisi za Mamlaka ili kutoa maelezo.

4.2 WAPO FM Radio ilieleza Mamlaka kuwa, wanakiri kosa kwa kushindwa kutafsiri na kutekeleza Kanuni ya 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) ,2018 pamoja na Masharti ya Leseni kwa kutangaza matangazo ya tiba asili na tiba mbadala ya Pelegrino Investment Sanitarium Clinic, Tesha Herbal Clinic & Natural Therapy, na Dr. Magida Traditional Medicine ambayo hayajaidhinishwa na TAHPC.

4.3 Kwamba, walifanya maamuzi ya kuingia kwenye mikataba na watoa huduma wa tiba asili na tiba mbadala tajwa kwa kuzingatia leseni zao walizowasilisha na zilizoonesha kuwa wamesajiliwa na TAHPC. Kupitia leseni hizo WAPO FM Radio ilikubali kutangaza biashara za watoa huduma hao, kwa kuamini kuwa TAHPC ilipowapa leseni ilijiridhisha, kuzitambua na kuzikubali huduma zao kuwa zinafaa kwa mlaji.

4.4 Wakiendelea kutoa utetezi wao, WAPO FM Radio walieleza Mamlaka kwamba, wametambua kinachotakiwa ili kutangaza biashara za tiba asili na tiba mbadala siyo leseni peke yake bali, ni kibali maalum kutoka kwa TAHPC cha kuidhinisha kufanya matangazo ya tiba hizo. WAPO FM Radio iliendelea kuieleza Mamlaka kuwa, wametii Amri ya Utekelezaji kwa kuwasimamisha rasmi wateja wao wote wanne (4) wanaotangaza tiba asili na tiba mbadala kuanzia tarehe 7 Januari 2024, na kuwataka wawasilishe kibali kutoka Mamlaka husika (TAHPC) ndipo wataendelea kupatiwa huduma ya kutangaza biashara zao.

4.5 Kuhusu kukaidi Maelekezo ya Mamlaka yaliyotolewa tarehe 5 Oktoba 2023 na tarehe 14 Novemba 2023, WAPO FM Radio ilieleza kuwa, haikuwahi kupokea barua zenye maelekezo hayo.

4.6 Katika kutoa maelezo zaidi kwa Mamlaka, WAPO FM Radio iliomba radhi kwa kutenda kosa hilo na kuahidi kutorudia tena, na kwamba watakuwa makini kutafsiri Kanuni ipasavyo ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na madhara au athari kwa Jamii. Hivyo, wanaahidi kutoa ushirikiano unaohitajika kwa Mamlaka na kwamba wataendelea kupata uelewa zaidi juu ya Sheria na Kanuni za Utangazaji.

## 5.0 UCHAMBUZI WA UTETEZI WA WAPO FM RADIO

Mamlaka imefanya uchambuzi na kuzingatia utetezi wa WAPO FM Radio kama ifuatavyo: -

5.1 WAPO FM Radio katika utetezi wao wa maandishi na mdomo, wamekiri kosa la kukiuka Kanuni ya 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) ,2018 pamoja na Masharti ya Leseni kwa kutangaza matangazo ya tiba asili na tiba mbadala ya Pelegrino Investment Sanitarium Clinic, Tesha Herbal Clinic & Natural Therapy, na Dr. Magida Traditional Medicine ambayo hayajaidhinishwa na TAHPC.

5.2 Utetezi wa WAPO FM Radio ni kwamba, wameshindwa kutafsiri Kanuni 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) ,2018 kwa sababu hawakuelewa kuwa kinachohitajika ni kibali cha matangazo ya tiba asili na tiba mbadala, badala yake walidhani leseni

peke yake inajitosheleza. Mamlaka imezingatia utetezi huo na kuona kuwa hauna msingi kwa kuwa, WAPO FM Radio kama Mtoa huduma ana wajibu wa kuelewa na kutekeleza Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni yake. Hata hivyo, kutokujua au kutokuelewa Sheria hakuwezi kuondoa au kufuta kosa linalotokana na ukiukwaji wa Sheria au Kanuni husika.

5.3 Mamlaka imerejea maelekezo na maagizo yaliyotolewa kwa WAPO FM Radio kuhusu utekelezaji wa Kanuni iliyoainishwa kwenye aya 5.1, katika barua ya tarehe 5 Oktoba 2023 na tarehe 14 Novemba 2023, ambapo maagizo hayo hayakutekelezwa. Kwa upande mwingine, Mamlaka imezingatia jitihada zilizochukuliwa na WAPO FM Radio katika kutekeleza agizo la Amri ya Utekelezaji la tarehe 4 Januari 2024, kwa kuwasimamisha rasmi wateja wao wote wanaotangaza tiba asili na tiba mbadala, na kuwataka wawasilishe kibali kutoka Mamlaka husika (TAHPC) ili waweze kuendelea kutangaza biashara zao.

5.4 Mamlaka pia imezingatia madhara na athari hasi kwa mlaji, ambazo zinaweza kusababishwa na tiba asili/mbadala kupitia matangazo ya tiba ambazo hazijaidhinishwa au kupewa kibali na Mamlaka husika ya TAHPC.

5.5 WAPO FM Radio wameomba radhi kwa Mamlaka kwa kutenda kosa na kuahidi kutorudia tena. Pia, wameahidi kutoa ushirikiano unaohitajika kwa Mamlaka na kwamba, watakuwa makini katika kutafsiri Kanuni ipasavyo, ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na madhara au athari kwa Jamii.

## 6.0 UAMUZI

6.1 **HIVYO BASI,** baada ya kusikiliza na kuzingatia utetezi wa WAPO FM Radio, Mamlaka imeona kwamba WAPO FM Radio **imekiuka** Kanuni ya 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018 pamoja na Masharti ya Leseni, kwa kuwa na mwenendo wa kutangaza matangazo ya watoa huduma za tiba asili na tiba mbadala ya ***Pelegrino Investment Sanitarium Clinic***, ***Tesha Herbal Clinic& Natural Therapy*** na ***Dr. Magida Traditional Medicine*** ambayo hayajaidhinishwa na TAHPC.

6.2 Kwa kuzingatia kifungu cha 114 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Sura ya 306, Marejeo ya 2022) na kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Sura ya 172 ya Sheria za Tanzania),

6.2.1. TCRA inaiagiza Wapo FM Radio kuacha kutangaza matangazo ya tiba asili na tiba mbadala yasiyozingatia Sheria na Kanuni;

6.2.2. Wapo FM Radio inaonywa kutorudia kukiuka Kanuni Kanuni ya 20 (1) (f) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Ikiwa WAPO FM Radio itakiuka, kupuuza au kukaidi AMRI hii ndani ya kipindi cha **miezi sita (6)** kutoka tarehe ya Uamuzi huu, Mamlaka itachukua hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti dhidi ya WAPO FM Radio, ikiwemo kutozwa faini, kusimamishiwa au kufutiwa leseni bila kutoa taarifa kwa WAPO FM Radio na kwa gharama za WAPO FM Radio.

Uamuzi huu umetolewa leo tarehe....09.......... **Februari 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Uamuzi huu umepokelewa na **WAPO FM Radio**, leo tarehe...10....... **Februari 2024.**

Jina ...Prince William...

Saini ..........................

Cheo/Wadhifa ...Secretary.....

(Muhuri)

10/02/2024
SATURDAY
12:33 MCHANA
0719021718

*(Uamuzi huu umetolewa katika nakala mbili (duplicate). Tafadhali weka saini katika nakala zote mbili na ubaki na nakala yako, kisha wasilisha nakala nyingine TCRA kuthibitisha kupokea Uamuzi.)*

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified